# Kituo kikubwa cha MNR chatekwa

U. 29-12-87

**MAPUTO, Msumbiji,**

**MSUMBIJI ilisema juzi kwamba majeshi yake yamekiteka kituo kikubwa cha magaidi cha MNR kilichoko kilomita 220 kaskazini mwa mji wa Maputo katika mkesha wa kuamkia siku kuu ya Krismasi.**

Gazeti la kila siku la Noticias lilisema kuwa kambi hiyo ya magaidi yenye nyumba 1,000 ilikuwa katika msitu mkubwa karibu na ziwa huko Nhalala karibu kilomita 160 mashariki ya mpaka wa Msumbiji na Afrika Kusini.

Gazeti hilo lilisema kuwa kituo hiki kilikuwa kinatumika kufanya mashambulizi kwenye njia kuu nchini Msumbiji ya kutoka kaskazini kwenda kusini. Watu wapatao 400 waliuawa katika mashambulizi yaliyofanyika Oktoba na Novemba mwaka huu katika eneo la kilomita 80 la mji wa Maputo. Serikali ya Msumbiji ilishutumu magaidi wa MNR kwa kuhusika na mashambulizi hayo.

Noticias ilisema kuwa magaidi 18 wa MNR waliuawa wakati wa mapigano yaliyofanyika kwenye kambi na wengine 1,000 walikimbia wengi wao wakiwa wamekimbilia upande wa Afrika Kusini.

Katika tukio lingine tofauti, mtu mmoja ambaye alijeruhiwa na kufanikiwa kufika salama nchini Swaziland aliwaambia waandishi wa habari kuwa aliwaona magaidi wakimmwagia dereva wa lori petroli na kumchoma moto wakati wa mashambulizi yaliyofanyika kwenye mpaka wa Swaziland mwishoni mwa wiki.

Maria Dlamini ambaye alipigwa risasi kwenye miguu na shingo aliwaambia waandishi wa habari kutoka hospitali alikolazwa mjini Mbabane kuwa magaidi wakiwa wamevaa nguo za jeshi walifyatulia risasi lori na kuwa watu watatu kati ya 10 waliokuwepo kwenye lori hilo huenda waliuawa.

Alisema kuwa waliwaamuru walionusurika kupakua mizigo iliyokuwa ndani ya lori, kummwagia dereva petroli na kumchoma moto. Gari lilipuka kutokana na moto.

Dlamini alisema kuwa yeye pamoja na rafiki yake walikimbia mwendo wa kilomita moja mpaka walipokutana na askari wa serikali ambao waliwapeleka Lomahasha, mji uliko kwenye mpaka.

Televisheni ya Maputo ilionyesha filamu ya mashambulizi hayo ya Nhalala na watazamaji waliona magaidi wakijibu mapigo ambapo gaidi mmoja aliuawa.